Swahili

# MWONGOZO WA WANAFUNZI WAPYA KWA MFUMO WA SHULE ZA KANADA

## KARIBU KANADA NA SHULE YAKO MPYA

Mwongozo huu utawasilisha taarifa muhimu kwa familia na wanafunzi wapya kuhusu mfumo wa shule za umma nchini Kanada. Taarifa ifuatayo itawapa wazazi/walezi ufahamu bora wa kile wanachopaswa kutarajia wakati wa elimu ya mtoto wao. Pia itatoa vidokezo vya kufaulu kwa wanafunzi na kuwasaidia wazazi/walezi kuwasiliana na shule ya mtoto wao. Mwongozo huu unakusudiwa kuwapa wanafunzi wapya muhtasari wa sera na taratibu za shule ili kusaidia mchakato wa uhamiaji.





SAISIA
Saskatchewan Association of Immigrant Settlement and Integration Agencies
Association des agences d'établissement et d'intégration des immigrants de la Saskatchewan

PNT SWIS Coordination
Maryam.Karimi@saisia.ca

# JEDWALI LA YALIYOMO


Mfumo wa Shule za Kanada................................................................. ukurasa 4
Shule za Umma ................................................................ ukurasa 4
Shule za Kibinafsi ................................................................ ukurasa 4

---

Gredi katika Mfumo wa Shule ................................................................ ukurasa 4
Shule za Awali ................................................................ ukurasa 4
Shule ya Msingi ................................................................ ukurasa 4
Shule ya kati na Shule ya Upili (Sekondari) ........................................ ukurasa 5

---

Taratibu za Shule ................................................................ ukurasa 5
Mwaka wa Shule ................................................................ ukurasa 5
Siku ya Shule ................................................................ ukurasa 6
Mahudhurio ................................................................ ukurasa 6
Kufungwa kwa Shule ................................................................ ukurasa 6
Kanuni ya Mavazi ................................................................ ukurasa 7
Kuweka Alama................................................................ ukurasa 7
Kadi za Ripoti ................................................................ ukurasa 7
Mahojiano baina ya Wazazi na Walimu ................................................ ukurasa 7
Mahitaji ya Shuleni ................................................................ ukurasa 8
Safari za nje ya Shule ................................................................ ukurasa 8
Nidhamu ya Wanafunzi ................................................................ ukurasa 8

---

Wajibu na Majukumu ................................................................ ukurasa 9
Waziri wa Elimu ................................................................ ukurasa 9
Bodi za Shule ................................................................ ukurasa 9
Mabaraza ya Shule ................................................................ ukurasa 9
Wakuu wa Shule ................................................................ ukurasa 9
Walimu ................................................................ ukurasa 10
Washauri Tabia wa Shule ................................................................ ukurasa 10
Wahudumu wa Kijamii Shuleni ................................................................ ukurasa 10
Walimu wa Kiingereza kama Lugha ya Pili ................................................ukurasa 10
Mpango wa Wafanyakazi wa Makazi Shuleni ........................................ ukurasa 11

# JEDWALI LA YALIYOMO

Ushiriki wa Wazazi: Kwa nini ni Muhimu? ............................... ukurasa 12
Inaboresha Mafanikio ya Wanafunzi ...................................... ukurasa 12
Hukuza Mawasiliano baina ya Wazazi na Shule ......................... ukurasa 12
Inakuza Ujenzi wa Uhusiano ................................................ ukurasa 12

---

Jinsi Wazazi Wanavyoweza Kuhusika ...................................... ukurasa 13
Jiunge na Baraza la Shule ................................................. ukurasa 13
Shiriki katika Shughuli za Shule ........................................... ukurasa 13
Kujitolea ....................................................................... ukurasa 13

---

Matarajio ya Wanafunzi ..................................................... ukurasa 14
Mahudhurio na Ushiriki Darasani .......................................... ukurasa 14
Kuwa Shuleni bila Kuchelewa ............................................... ukurasa 14
Kazi ya Ziada ................................................................. ukurasa 15
Matumizi ya Simu za rununu/Mtandao .................................... ukurasa 16
Miongozo ya Tabia ........................................................... ukurasa 16

---

Taarifa Nyingine ............................................................. ukurasa 17
Shughuli za Ziada ............................................................ ukurasa 17
Uchaguzi wa Kozi za Shule ya Sekondari ................................. ukurasa 18
Mzio .............................................................................. ukurasa 18
Marejeleo ....................................................................... ukurasa 19-20

## Mfumo wa Shule za Kanada

Nchini Kanada, hakuna idara ya elimu ya serikali ya shirikisho; kila mkoa/eneo linawajibika kwa mfumo wake wa shule, Wizara ya Elimu (Ministry of Education), na Sheria ya Elimu (Education Act). Sheria ya Elimu ni kifungu cha sheria ambacho kinaainisha mamlaka na wajibu wa Wizara ya Elimu, Bodi za Shule Wakuu wa Shule na Walimu. Waziri wa Elimu ni mjumbe aliyechaguliwa na serikali ya mkoa, na kila mkoa una Waziri wake ambaye anateuliwa na Waziri Mkuu wa mkoa. Mfumo wa shule nchini Kanada unajumuisha shule za umma na za kibinafsi.

## Shule za Umma

Shule za umma zinatoa elimu bila malipo ambayo hugharamiwa na serikali. Mbali na shule zinazofundishwa kwa Kiingereza, mfumo wa shule za umma unajumuisha:

- Shule za Kuzamisha za Kifaransa
  - Kwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza si Kifaransa
- Shule za Lugha ya Kifaransa
  - Kwa watoto walio na angalau mzazi mmoja ambaye ni mzungumzaji Asilia wa Kifaransa

Huko Albata (Alberta), Saskachewan (Saskatchewan), na Ontario, Shule za Kikatoliki pia zimejumuishwa katika mfumo wa shule za umma.

## Shule za Kibinafsi

Shule za kibinafsi ni shule ambazo hazifadhiliwi (au hazifadhiliwi kikamilifu) na serikali. Kwa sababu hiyo, wanatoza ada ya masomo kwa wanafunzi wanaotaka kuhudhuria

## Gredi katika Mfumo wa Shule

### Shule za Awali

Shule za Awali (Preschool) ni fursa ya hiari ya elimu kwa watoto wenye umri wa miaka 3-5, kabla ya kuanza elimu yao ya lazima. Shule za Awali huzingatia zaidi masomo ya mapema na masomo kuliko shule za watoto (daycare) na zinaweza kuwatayarisha watoto kwa miaka yao ya shule.

## Gredi katika Mfumo wa Shule

### Shule ya Msingi

Shule ya msingi inajumuisha chekechea na darasa la 1 hadi 6. Nchini Kanada, ni lazima kwa watoto kuanza kuhudhuria shule wakiwa na umri wa miaka 6, au Darasa la 1. Vighairi pekee kwa hili ni British Columbia, Prince Edward Island, na New Brunswick, ambapo ni lazima kwa watoto kuanza shule wakiwa na umri wa miaka 5, au chekechea. Ingawa shule ya chekechea ni ya hiari katika mikoa mingine, wazazi wanahimizwa kuwaandikisha watoto wao katika shule ya chekechea kwani inasaidia watoto kukuza ujuzi wa kutatua matatizo na ustadi baina ya watu.

## Gredi katika Mfumo wa Shule

### Shule ya kati na Shule ya Upili (Sekondari)

Katika baadhi ya mikoa/maeneo, shule ya kati inajumuisha darasa la 7 na 8, huku shule ya upili ikijumuisha darasa la 9-12. Katika Kibeki (Quebec), shule ya upili inajumuisha darasa la 7-12.

Mikoani, wazazi wanahimizwa kuwasajili watoto wao katika shule ya chekechea kwani husaidia watoto kukuza ustadi wa kutatua shida na ustadi wa kibinafsi.

## Taratibu za Shule

### Mwaka wa Shule

Mwaka wa shule unaanza mwishoni mwa Agosti au Septemba mapema hadi mwishoni mwa Mei au mapema Juni. Wanafunzi basi wana likizo ya majira ya joto (summer) kutoka Juni hadi Agosti. Shule hufungwa kwa likizo zote za kisheria, mapumziko ya majira ya baridi (winter) mwishoni mwa Desemba, na mapumziko ya (spring) mwezi Machi au Aprili. Kunaweza pia kuwa na siku kadhaa mwaka mzima ambapo wanafunzi hawana shule kwa sababu walimu wana siku za maendeleo ya kitaaluma au siku za kufanya mipango. Kila shule itakuwa na kalenda ambayo itaonyesha siku ambazo ni likizo au siku za kupumzika kwa mwaka wa shule.



Nchini Kanada, ni kwa mujibu wa sheria kwamba watoto wahudhurie shule kutoka umri wa miaka 6-16 (18 katika baadhi ya mikoa)

## Siku ya Shule

Shule huanza Jumatatu hadi Ijumaa na kwa kawaida huanza kati ya 8:00 na 9:00 asubuhi na kumaliza kati ya 3:00 na 4:00 jioni. Angalau mapumziko mawili ya dakika 15, au mapumziko katika shule ya msingi, na mapumziko ya saa moja wakati wa chakula cha mchana hutolewa wakati wa mchana. Wazazi wana wajibu wa kumpa mtoto wao chakula cha mchana kilichopakiwa ikiwa hawezi kwenda nyumbani wakati wa saa ya chakula cha mchana. Shule zingine zina mikahawa ambapo chakula cha mchana kinaweza kununuliwa.

## Kufungwa kwa Shule

Katika tukio la hali mbaya ya hewa (mfano hali ya theluji) shule zinaweza kufunga au kufukuza wanafunzi mapema kwa usalama wa wanafunzi na wafanyikazi. Wazazi/walezi watafahamishwa kuhusu kufungwa kwa shule au kufukuzwa mapema na watawajibika kumchukua mtoto wao kutoka shuleni ikiwa hawataweza kutumia basi kwenda nyumbani. Huduma za basi za shule pia zinaweza kughairiwa wakati wa hali mbaya ya hewa. Wazazi/walezi wana jukumu la kufuatilia huduma za basi na kupanga usafiri mbadala ikiwa mabasi yameghairiwa ili watoto wao wafike shuleni salama.

## Mahudhurio

Wanafunzi wanatarajiwa kuhudhuria, na kuwa darasani kwa wakati ufaao, madarasa yote. Ikiwa mwanafunzi hataweza kuhudhuria, mzazi/mlezi huwajibika kupiga simu shuleni na kuwafahamisha sababu ya kutokuwepo kwa mtoto wao. Sababu zinazokubalika za kutokuwepo ni pamoja na:

- Ugonjwa
- Sababu za huruma (compassionate reasons)
- Miadi ya matibabu/meno
- Sababu za mahakama/kisheria

Ikiwa mwanafunzi hayupo shuleni kwa zaidi ya siku mbili, wazazi/walezi wanapaswa kuwasiliana na ofisi ya shule na kuomba kazi ya ziada (homework) ambayo mtoto wao anaweza kukosa wakati wa kutokuwepo kwake.



## Mavazi kwa ajili ya Hali ya Hewa

Wanafunzi wa shule ya msingi mara nyingi hucheza nje wakati wa mapumziko na chakula cha mchana, isipokuwa wakati wa hali mbaya ya hewa. Wazazi/walezi lazima wahakikishe kwamba mtoto wao amevaa vizuri kulingana na hali ya hewa. Koti ya baridi, glavu, kofia, na buti ni muhimu wakati wa miezi ya baridi.

## Kanuni ya Mavazi

Kila shule itakuwa na sera yake inayoeleza wanafunzi wanachoruhusiwa/wasichoruhusiwa kuvaa shuleni. Wanafunzi wanatarajiwa kufuata kanuni za mavazi za shule zao.

## Kuweka Alama

Walimu watatathmini kazi na ujifunzaji wa kila mwanafunzi, na kutoa daraja la herufi katika kozi, kulingana na tathmini yao. Baadhi ya njia ambazo walimu huwatathmini wanafunzi ni pamoja na:

- Maswali na mitihani
- Ripoti zilizoandikwa au za kusemwa
- Kazi ya ziada (homework)
- Miradi ya wanafunzi
- Ushiriki darasani
- Kazi za kila siku

## Kadi za Ripoti

Wanafunzi watapokea kadi za ripoti katika mwaka mzima wa shule na alama zao katika kila kozi kulingana na za mwalimu aliyetathmini. Mara nyingi yatajumuisha maoni kutoka kwa walimu kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Kadi za ripotizinatarajiwa kukaguliwa na kusainiwa na wazazi/walezi na kurudishwa shuleni.

## Mahojiano baina ya Wazazi na Walimu

Mahojiano ya Wazazi na Walimu (Parent-Teacher Interviews) ni mikutano iliyoratibiwa kati ya wazazi/walezi na walimu wa mtoto wao. Yatatokea katika maeneo tofauti kwa mwaka mzima wa shule na kuruhusu wazazi/walezi kujadili kuhusu maendeleo ya ujifunzaji na elimu ya mtoto wao. Wakati wa mikutano hii, walimu wanaweza kushiriki kazi ya mtoto na kujadili mafanikio yao na wazazi/walezi. Walimu wanaweza pia kujadili matatizo waliyo nayo na kufanya kazi na wazazi kutafuta suluhu.



**Mifumo ya Kukadiria matokeo Itatofautiana kidogo kati ya mikoa, lakini kwa ujumla, fuata hii umbizo:**

A=80-100% (Bora sana)
B=70-79% (Nzuri)
C=60-69% (Wastani)
D=50-59% (Mbovu)
F=0-49% (Amefeli)

## Mahitaji ya Shuleni

Wazazi/walezi wana wajibu wa kutoa vifaa vya msingi vya shule kwa watoto wao. Shule nyingi zitatoa orodha ya vifaa vya shule ambavyo wanafunzi watahitaji kuja navyo. Vitabu vya kiada hutolewa na shule, na wanafunzi wanaweza kupata nyenzo zingine za kusoma kutoka kwa maktaba ya shule yao. Wanafunzi wanaweza kuhitajika kuwa na jozi tofauti ya viatu vinavyofaa kwa madarasa ya michezo na mazoezi.

## Safari za nje ya Shule

Safari za nje ya shule (Filed Trips) ni safari maalum za darasa za kutembelea maeneo kama makumbusho, sinema, vituo vya sayansi au mashamba ili kupata elimu na uzoefu nje ya darasa. Safari hizi hupangwa na walimu, na mwanafunzi atatumwa barua awasilishe nyumbani ili kuwajulisha wazazi/walezi kuhusu safari hiyo. Sahihi kutoka kwamzazi/mlezi itahitajika ili kutoa ruhusa mwanafunzi kuhudhuria safari hiyo. Kunaweza kuwa na fursa kwa wazazi kujitolea kumsaidia mwalimu katika safari hizi.

## Nidhamu ya Wanafunzi

Tabia ya kuvuruga na kutoheshimu, au kushindwa kufuata sera za shule (kama vile sera za mahudhurio au kanuni za mavazi) kunaweza kusababisha hatua za kinidhamu. Walimu mara nyingi watashughulikia matukio madogo na mwanafunzi, lakini tabia isiyofaa ikiendelea, kutahitajika mkutano na wazazi/walezi wa mwanafunzi huyo. Usimamizi wa shule pia unaweza kuhusika. Hatua za kinidhamu zinaweza kuwa ni pamoja na maonyo yaliyoandikwa, kuwekwa kizuizini, au kusimamishwa shule kwa muda (suspension). Wazazi/walezi wafaa washirikiane na walimu pale masuala ya tabia ya kuvuruga au kushindwa kufuata sera za shule yanapoibuliwa na walimu. Wazazi/walezi wanaweza kuzungumza na mwalimu kuhusu tabia ya mtoto wao na kufanya kazi pamoja kutafuta suluhu. Wazazi/walezi wanaweza pia kuzungumza na washauri wa tabia wa shule.



## Hatua za Nidhamu kwa Watoro

- Kwanza, simu itapigwa kwa mzazi/mlezi kutoka kwa mwalimu.
- Baada ya kutokuwepo mara nyingi, simu itapigwa kwa mzazi/mlezi kutoka kwa mshauri wa tabia wa au Msimamizi wa shule.
- Ikiwa kutokuwepo kutaendelea, mkutano na mwanafunzi, mzazi/mlezi, na mshauri au msimamizi unaweza kuwa umepangwa.
- Tatizo likiendelea, mwanafunzi anaweza kuondolewa kwenye kozi.

**Wazazi na wanafunzi wanapaswa kufahamu sera mahususi ya mahudhurio ya shule zao, kwani taratibu za shule zinaweza kutofautiana kati ya shule.*

## Wajibu na Majukumu

### Waziri wa Elimu

Waziri wa Elimu (Minister of Education) ana jukumu la kuandaa sera na mitaala ya elimu, kuweka miongozo ya shule kwa wakuu na bodi za shule, na kuandaa orodha za nyenzo za kujifunzia zilizoidhinishwa. Pia wana jukumu la kusimamia fedha kwa bodi za shule.

## Wajibu na Majukumu

### Bodi za Shule

Bodi za Shule (School Boards) zinahusisha Wadhamini ambao huchaguliwa katika chaguzi za manispaa. Bodi za shule zina jukumu la kutenga fedha zinazotolewa kwao na Waziri wa Elimu. Pia wana wajibu wa kusimamia uendeshaji wa shule, kuajiri wafanyakazi, na utendaji wa walimu. Bodi za shule huhakikisha programu za ufundishaji za hali ya juu zinazoakisi mahitaji na maadili ya jamii.

## Wajibu na Majukumu

### Mabaraza ya Shule

Mabaraza ya Shule (School Councils) yanahusisha wazazi, wanajamii, wakuu wa shule, walimu na wanafunzi wa sekondari. Mabaraza ya shule hutoa mapendekezo kwa mkuu au bodi ya shule kuhusu mtaala, utendaji wa shule na mahitaji ya kujifunza. Wanaweza pia kushauri kuhusu uteuzi wa wakuu wa shule, matumizi ya shule na jamii, na sera ya bodi ya shule.

## Wajibu na Majukumu

### Wakuu wa Shule

Wakuu wa shule wana jukumu la kusimamia ushirika na usimamizi wa shule zao. Wakuu wa shule husimamia bajeti ya shule, husimamia wafanyakazi wa shule, na kutoa mapendekezo kwa bodi ya shule kuhusu kupandishwa cheo au kufukuzwa kazi kwa walimu.

**Bodi za shule hufanya mikutano mara kwa mara ambayo huwa wazi kwa umma. Hii inawapa wenyeji fursa ya kutoa maoni na wasiwasi wao kuhusu elimu katika jamii zao.**

## Wajibu na Majukumu

### Walimu

Walimu wana wajibu wa kuunda mipango ya masomo na madarasa ya kufundisha. Walimu hutathmini maendeleo ya wanafunzi na kuwasaidia wanafunzi kwa mipango ya elimu na malengo ya kazi. Walimu pia wana wajibu wa kuwasimamia wanafunzi na kudumisha nidhamu katika madarasa yao.

## Wajibu na Majukumu

### Washauri Tabia wa Shule

Washauri Tabia wa Shule (School Counsellors) wana jukumu la kukuza afya ya akili na kusaidia wanafunzi ambao wanakabiliwa na shida. Watafanya kazi na watu binafsi na vikundi kuhusu masuala mbalimbali kama vile matumizi mabaya ya dawa za kulevya, uonevu, udhibiti wa hasira, na mafadhaiko na wasiwasi. Washauri tabia wa shule wanaweza kuunganisha wanafunzi na familia kwa usaidizi mwingine katika jamii. Washauri tabia wa shule pia hutoa ushauri juu ya uteuzi wa kozi na kupanga kazi.

## Wajibu na Majukumu

### Wahudumu wa Kijamii Shuleni

Wahudumu wa Kijamii Shuleni (School Social Workers) hutoa ushauri kwa mtu binafsi, familia, na vikundi na kuunganisha wanafunzi na familia kwa rasilimali za jamii inapohitajika. Wanahimiza ushiriki wa wazazi katika maisha ya shule na kutoa programu za elimu kwa wazazi na wafanyikazi wa shule. Wahudumu wa Jamii wa Shule pia hutoa usaidizi kwa wanafunzi wanaoshughulikia migogoro ya kifamilia, kutojithamini, mahusiano, kujamiiana, matatizo ya kujifunza na masuala ya afya ya akili.

## Wajibu na Majukumu

### Walimu wa Kiingereza kama Lugha ya Pili

Walimu wa Kiingereza kama Lugha ya Pili (English as a Second Language – ESL) hutoa maelekezo ya lugha maalum kwa wanafunzi ambao hawazungumzi Kiingereza kama lugha yao ya kwanza. Wanatathmini ustadi wa lugha wa wanafunzi wapya na programu za kubuni ili kukidhi mahitaji ya lugha ya mtu binafsi. Walimu wa Kiingereza kama Lugha ya Pili wanaweza kubuni mipango ya somo kuhusu shughuli zinazohusika katika maisha ya kila siku nchini Kanada, na utamaduni wa Kanada.

## Tathmini ya Lugha

Kiwango cha Kiingereza cha mtoto wako kitatathminiwa wanaposajiliwa shuleni. Tathmini hii ya lugha itasaidia shule kuamua ni kiasi gani cha ziada Msaada wa Kiingereza kama lugha ya pili wanaohitaji.

## Wajibu na Majukumu

### Mpango wa Wafanyakazi wa Makazi Shuleni

Mpango wa Wafanyakazi wa Makazi Shuleni (Settlement Workers in Schools Program – SWIS) ni huduma ya makazi shuleni inayofadhiliwa na idara ya Uhamiaji, Wakimbizi, na Uraia nchini Kanada (Immigration, Refugees, and Citizenship Canada – IRCC) na inapatikana katika kila mkoa. Watoa huduma za makazi huweka wafanyikazi wa makazi katika shule zinayo idadi kubwa ya wanafunzi wapya. Wafanyakazi wa SWIS hushirikiana na shule, mashirika ya jamii, na watoa huduma za makazi ili kuwasaidia wanafunzi wapya na familia zao kukaa shuleni mwao. Malengo ya programu za SWIS ni kukidhi mahitaji ya wanafunzi wapya na familia na kuwasaidia katika kupokea huduma zinazohitajika ili kufaulu. Baadhi ya malengo ya programu ni kwamba wanafunzi na familia wana ujuzi kuhusu na kushikamana na shule zao, kwamba wamefaulu shuleni mwao, na kwamba wanahisi kuungwa mkono na kuwezeshwa.

**Jinsi Wafanyikazi wa SWIS Wanaweza Kukusaidia**

- Usaidizi wa usajili wa shule, mwelekeo, na mahojiano ya wazazi na walimu
- Kutoa taarifa muhimu kwa wazazi/walezi na wanafunzi kuhusu sera za shule, matarajio, sheria, na shughuli za ziada
- Kutathmini mahitaji na kutoa rufaa na miunganisho kwa rasilimali za jumuiya
- Kuongeza ushiriki wa familia katika jamii kwa kuwaelekeza kwenye programu za jamii zinazoweza kumudu
- Kuongeza ushiriki wa wazazi katika elimu na kukuza mawasiliano kati ya wazazi na wafanyakazi wa shule
- Kuhakikisha wazazi/walezi na wanafunzi wanafahamu haki na wajibu wao na wanatetea haki za wanafunzi na familia zao
- Kutoa hudumaza masuala nyeti ya kitamaduni na kukuza heshima kwa tofauti za kitamaduni ndani ya shule na jamii kupitia vipindi vya elimu
- Kushirikiana na wafanyakazi wa shule na washauri wa shule ili kutoa afua zenye uwezo wa kiutamaduni katika nyakati za mgogoro
- Kutoa tafsiri na ukalimani

# Ushiriki wa Wazazi: Kwa nini ni Muhimu?

## Inaboresha Mafanikio ya Wanafunzi

Wazazi/walezi wanapohusika katika elimu ya mtoto wao inasisitiza thamani njema kwenye elimu na kuwahimiza wanafunzi na kuwahamasisha zaidi.

## Inakuza Ujenzi wa Uhusiano

Ushiriki wa wazazi pia unajumuisha uwepo katika shule ya mtoto. Wazazi/walezi wanaweza kukuza uhusiano na wafanyakazi wa shule, kuungana na wazazi wengine na kusaidiana, na kupata fursa ya kukutana na wanajamii au majirani.

## Hukuza Mawasiliano baina ya Wazazi na Shule

Ushiriki wa wazazi katika elimu ni pamoja na kufahamiana na wafanyakazi wa shule katika shule ya mtoto. Wazazi na wafanyakazi wa shule wanapofahamiana, inaruhusu mawasiliano ya njia mbili yenye ufanisi zaidi. Mawasiliano bora yanaweza kuifanya iwe rahisi kwa wazazi/walezi kuwafikia wafanyakazi wa shule wakiwa na wasiwasi au mahitaji.



## Jinsi Wazazi Wanavyoweza Kuwa na Habari Wakati Wote

- Mkumbushe mtoto wako unataka kuona taarifa kutoka shuleni, na umwombe mara kwa mara aangalie mkoba wake kwa matangazo au barua
- Angalia tovuti ya shule kwa taarifa mpya
- Angalia kalenda ya shule kwa orodha ya siku au matukio muhimu
- Wasiliana na ofisi ya shule na umwachie ujumbe mwalimu wa mtoto wako ikiwa una maswali

# Jinsi Wazazi Wanavyoweza Kuhusika

## Jiunge na Baraza la Shule

Kama wajumbe wa baraza la shule (school council), wazazi/walezi wana fursa ya kushirikishwa katika kufanya maamuzi ya shule. Pia, inaruhusu wazazi/walezi kushauri kuhusu programu za shule na fursa za kujifunza.



## Shiriki katika Shughuli za Shule

Wazazi/walezi wanaweza kuhusika kwa kuhudhuria michezo ya shule, matamasha, na matukio ya michezo, na kwa kwenda/kushirikikatika matukio ya jumuiya na mikutano inayoandaliwa na shule au baraza la shule. Wazazi/walezi pia wahudhurie mahojiano ya wazazi na walimu yote na wanahimizwa kuhudhuria mikutano ya bodi ya shule ili kuwa na habari kuhusu elimu ya mtoto wao.

## Kujitolea

Njia nyingine ya wazazi/walezi kushiriki katika elimu ya mtoto wao ni kujitolea huko shuleni. Baadhi ya walimu wa shule za msingi wanawahimiza wazazi kujitolea kusaidia katika madarasa yao. Wazazi/walezi wanaweza pia kujitolea kusaidia walimu kwa safari za nje ya darasa (field trips) au kusaidia hafla za kuchangisha pesa za shule.

## Jinsi Wazazi/Walezi Wanavyoweza Kukuza Mtazamo Mwema Kuhusu Elimu

- Kuhimiza ustahimilivu, uundaji wa malengo/mipango, na umuhimu wa kuomba msaada inapohitajika
- Kutoa nafasi tulivu kwa ajili ya kazi za ziada (homework)
- Kuonyesha shauku kwa programu na shughuli za shule
- Kusoma pamoja na watoto wako
- Kuuliza maswali mahususi kuhusu siku ya mtoto wako, shughuli za shule na kile anachojifunza



# Matarajio ya Wanafunzi

## Mahudhurio na Ushiriki Darasani

Wanafunzi wanatarajiwa kuhudhuria madarasa yote. Ikiwa mwanafunzi hatakuwepo darasani, lazima apate ruhusa kutoka kwa wazazi/walezi wao. Wanafunzi pia wanawajibika kwa kazi yoyote au majaribio ambayo wamekosa wakati wa kutokuwepo kwao. Sio tu wanafunzi kuhudhuria madarasa mara kwa mara, lakini pia wanatarajiwa kuwa washiriki wema katika madarasa yao. Hii ina maana kwamba walimu huhimiza na kutarajia wanafunzi kuuliza maswali, kufikiri kwa kina, na kutoa maoni yao juu ya mada zinazowasilishwa darasani. Ushiriki darasani unaweza kujumuisha kazi ya kikundi, ambapo wanafunzi wamegawanywa katika vikundi vidogo ili kujadili mada maalum na kisha wawasilishe mjadala wao kwa wanafunzi wengine. Wanafunzi wanaweza pia kutumwa kwa kikundi kukamilisha mradi au kazi ya ziada. Kila mwanafunzi anatarajiwa kuchangia kwa usawa katika zoezi hilo. Kazi ya kikundi ni muhimu kwa kufundisha wanafunzi kushirikiana wenyewe kwa wenyewe.

### Kwa Nini Kuhudhuria Ni Muhimu?

- Wanafunzi ambao hawaendi shuleni kwa muda mrefu wana uwezekano mkubwa wa kuacha shule
- Huwafundisha wanafunzi ujuzi wanaohitaji ili wafanikiwe baada ya kuhitimu
- Kutokuwepo kunaweza kusababisha wanafunzi kukosa masomo muhimu katika maudhui ya kozi na taarifa muhimu kuhusu kazi za darasani na mitihani
- Kutokuwepo shule mara mingi kunaweza kusababisha wanafunzi kurudi nyuma na kuwa na ugumu wa kusalia katika njia njema ya kuhitimu
- Ni muhimu kwa ajili ya kujenga uhusiano na wanafunzi wengine na kujenga hisia ya kujumuika

## Kuwa Shuleni bila Kuchelewa

Ni muhimu kwa wanafunzi kufika mapema kwa madarasa yao yote. Kuchelewa kufika darasani kunaweza kuwasumbua sana walimu na wanafunzi wengine. Mwanafunzi akichelewa darasani, atatarajiwa kupiga ripoti kwenye ofisi ya shule yake. Shule zingine zinaweza kuhitaji mwanafunzi kupata hati ya kuchelewa iliyosainiwa na mwalimu wake na kuirudisha ofisini. Ikiwa mwanafunzi anachelewa kwa darasa kila wakati, hatua za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa. Wazazi/walezi wahakikishe watoto wao wanapata usingizi wa kutosha ili kuhakikisha kwamba anaweza kuamka na kuwa na muda wa kutosha kujiandaa kwa ajili ya shule.


# Matarajio ya Wanafunzi

## Kazi ya Ziada

Wanafunzi wanatarajiwa kukamilisha kazi zote za ziada walizopewa kwa wakati na kwa uwezo wao wote. Wanafunzi wanaweza kupoteza alama kwa kupeana kazi za ziada kwa kuchelewa. Walimu wanaweza kupeana idadi maalum ya kurasa katika riwaya au kitabu cha kiada cha kusomwa kabla ya darasa lao linalofuata. Wanafunzi pia wanaweza kutarajiwa kukamilisha kazi zilizoandikwa au kujiandaa kwa mawasilisho ya mdomo kwa tarehe maalum. Wanafunzi wanapaswa kuandika kazi zote na tarehe za kukamilisha katika mpangaji wa siku ili kufuatilia kazi ya ziada na kuhakikisha kazi inakamilika kwa wakati ufaao.

## Vidokezo vya Kazi ya Ziada/Masomo

- **Tafuta mahali palipotulia pa kufanya kazi, palipo na vikengeushio vichache**
- **Kusikiliza na kuandika maelezo darasani kutakusaidia unaposoma**
- **Tumia mpangilio kuandika kazi na mitihani yote na kupanga muda wa kusoma/kufanya kazi za ziada**
- **Usiahirishe; kagua madokezo mara kwa mara ili kuepuka kubania mtihani usiku uliotangulia**






# Matarajio ya Wanafunzi

## Matumizi ya Simu za rununu/Mtandao

Utumiaji wa simu za rununu wakati wa darasa unaweza kuwasumbua wanafunzi wakati wa kujifunza, na kuwasumbua sana wanafunzi wengine. Shule nyingi zinatarajia wanafunzi kuepusha kutumia simu zao za rununu wakati wa darasa, na walimu wanaweza kuchukua simu kwa muda ikiwa wanafunzi hawafuati matarajio ya shule. Ikiwa mwanafunzi anatarajia simu muhimu, anapaswa kumjulisha mwalimu wake mapema. Shule nyingi pia zitatarajia wanafunzi kutumia kompyuta zao na mtandao kwa madhumuni ya elimu pekee. Wanafunzi wanaokiuka sera za matumizi ya mtandao au kufikia nyenzo zisizofaa wanaweza kuadhibiwa. Kila shule itakuwa na sera yake kuhusu matumizi ya simu za mkononi na mtandao na wanafunzi, pamoja na wazazi/walezi, wanapaswa kujifahamisha na sera ya shule yao.

## Miongozo ya Tabia

Shule zinapaswa kuwa sehemu salama zisizo na aina yoyote za ubaguzi, uonevu, na unyanyasaji. Kila shule itakuwa na kanuni zake za maadili na miongozo ya kitabia, inayoeleza matarajio ya wanafunzi wote kuhimiza na kukuza mazingira salama na yanayokubalika. Uonevu hutokea wakati mwanafunzi, au kikundi cha wanafunzi kinamtisha, au kumlazimisha mtu anayelengwa. Hii inaweza kujumuisha madhara ya kimwili, kisaikolojia, kijamii na kihisia. Wanafunzi, pamoja na wazazi/walezi, wanahimizwa kuripoti wasiwasi wowote kuhusu uonevu, unyanyasaji, au ubaguzi kwa mfanyikazi wa shule. Utawala wa shule unachukua unyanyasaji na ubaguzi kwa uzito. Wanafunzi wanaojihusisha na tabia ya ubaguzi na kutoheshimu wanafunzi wenzao watatarajiwa kukutana na washauri tabia wa shule au wafanyakazi wengine wa shule ili kutatua mzozo huo. Ikiwa tabia isiyofaa itaendelea, mwanafunzi anaweza kusimamishwa shuleni au kufukuzwa.





# Matarajio ya Wanafunzi

## Uonevu Mtandaoni (Cyber Bullying)

Ni matumizi ya simu za rununu, kompyuta, au vifaa vingine vya kielektroniki ili kunyanyasa, kutishia, kudhihaki au kuwa na ujeuri.kwa mtu mwingine mtandaoni.



Wanafunzi wanapaswa kuripoti barua pepe, maandishi, picha au ujumbe wowote unaowafanya waogope au kutokuwa na raha kwa mtu mzima anayeaminika au mfanyakazi wa shule.




Wazazi/walezi wanapaswa kufahamu programu ambazo watoto wao wanatumia, kuzungumza na watoto wao kuhusu uonevu mtandaoni, na wahakikishe watoto wao wanajua kuwa wapo ili kusikiliza ikiwa wanahitaji msaada.

## Taarifa Nyingine

### Shughuli za Ziada

Shughuli za ziada ni pamoja na michezo, sanaa, ukumbi wa michezo, muziki na vilabu vinavyofanyika nje ya saa za shule. Wanafunzi wanahimizwa kujiunga na timu, shughuli, au klabu inayowavutia. Kunaweza kuwa na ada zinazohusika na baadhi ya shughuli. Kama wazazi/walezi wana wasiwasi wowote kuhusu ada, wanapaswa kuzungumza na shule.



Kujihusisha na shughuli za ziada ni njia nzuri kwa wanafunzi kuhusika zaidi katika shule yao, kukutana na watu wapya, kujifunza jinsi ya kushirikiana na wengine, na kujenga ujuzi mpya.

# Matarajio ya Wanafunzi


## Uchaguzi wa Kozi za Shule ya Sekondari

Shule za upili zitakuwa na vijitabu vinavyopeanwa bila malipo ambavyo vinaeleza kozi zote zinazotolewa shuleni. Kuhitimu, wanafunzi watahitaji kukamilisha idadi ya masaa kwa kila somo (credits) inayotakiwa , kulingana na viwango vyao vya mkoa. Baadhi ya idadi ya masaa kwa kila somo itapatikana kutokana na kufaulu kozi za lazima, na iliyobaki itapatikana kutokana na kufaulu kozi za kuchaguliwa, ambazo mwanafunzi atachagua.

Programu za baada ya sekondari mara nyingi huhitaji madarasa fulani ya shule ya upili kukamilika (pia huitwa sharti) kwa wanafunzi kujiandikisha katika programu hizo. Wanafunzi wa shule ya upili wanaotaka kutuma ombi la kujiunga na shule ya upili wanahitaji kufahamu kozi watakazohitaji kuchukua. Ni muhimu kwa wanafunzi kukutana na mshauri wa mwongozo wa shule ambaye anaweza kuwasaidia na uteuzi wao wa kozi.

## Mzio

Baadhi ya watoto wana mizio (allergies) mikali ya kokwa (nuts) na watakuwa wagonjwa sana ikiwa watapata chakula chenye karanga (hata kiasi kidogo sana). Wazazi/walezi watafahamishwa iwapo shule ina wanafunzi wenye mzio wa kokwa na kupewa habari kuhusu jinsi shule inavyoshughulikia suala hilo. Wazazi/walezi wanaweza kuombwa wasitume watoto wao chakula chochote kilicho na kokwa au karanga. Ikiwa mtoto wako ana mzio mkali au tatizo lingine la afya, unapaswa kuhakikisha kuwa shule inafahamu ya suala hilo.





# MAREJELEO


Anaphylaxis law and policies by province and territory retrieved from: https://foodallergycanada.ca/professionalresources/educators/school-k-to-12/nationalschool-policies/

Be Here retrieved from: https://www.spsd.sk.ca/division/behere/Pages/default.aspx#/=

Council of Ministers of Education, Canada retrieved from: https://www.cmec.ca/299/education-in-canada-anoverview/index.html

Cyber Safety Tips retrieved from: https://bekindonline.com/category/cyber-safetytips/

Education Act retrieved from: https://www.alberta.ca/educationguide-education-act.aspx

Education in Canada: Life in Canadian Schools retrieved from: https://www.canada.ca/en/immigration-refugeescitizenship/services/newimmigrants/new-lifecanada/education/how-it-works.html

Education in Canada: Types of Schooling retrieved from: https://www.canada.ca/en/immigration-refugeescitizenship/services/newimmigrants/new-lifecanada/education/types-school.html

English Language Assessment retrieved from: https://www.spsd.sk.ca/registration/noncanadian/NSC/ELA/Pages/default.aspx#/=

ESL Teachers retrieved from: https://pwp.vpl.ca/siic/guides/eslteachers/

Extracurricular Activities retrieved from:https://www.saskatoonpublicschools.ca/school/evanhardy/ProgramsServices/extracurr/Pages/default.aspx#/=

Help protect your child from cyberbullying retrieved from: https://www.canada.ca/en/publicsafety-canada/campaigns/cyberbullying/helpprotect-your-child-from-cyberbullying.html

Key Roles of SWIS retrieved from: https://swissask.ca/about-us/

Kindergarten is Optional Depending on Where You Live retrieved from: https://globalnews.ca/news/4056554/kindergarten-is-optional-depending-on-where-you-live/

Learning & Education retrieved from: https://kidshealth.org/en/parents/positive/#catlearning

Parent Engagementretrieved from: http://www.edu.gov.on.ca/eng/parents/involvement/

The State of High School Guidance Counselling in Canada retrieved from: https://canadianschoolcounsellor.com/winter2018/winter2018-features/the-state-of-highschoolguidance-counselling-in-canada/

Who's responsible for your child's education? retrieved from: http://www.edu.gov.on.ca/eng/document/brochure/whosresp.html#minister

# MAREJELEO


Parent-Teacher Interviews retrieved from: https://settlement.org/ontario/education/elementary-and-secondary-school/help-your-childsucceed-in-school/parent-teacher-interviews/

Progressive Discipline retrieved from: http://www.edu.gov.on.ca/eng/safeschools/discipline.html

Public Education in Canada retrieved from: https://www.cdnsba.org/all-about

Settlement Services provided by Settlement Workers in Schools (SWIS) retrieved from: https://www.eisaedmonton.org/services/settlementservices/community-settlement-services/

Settlement Workers in Schools Best Strategies: Step-by-Step Activity Guidelines Manual retrieved from: https://swissask.ca/wpcontent/uploads/2019/12/best-strategies-step-bystep-activity-guidlines.pdf

Severe Weather retrieved from: https://www.spsd.sk.ca/division/severeweather/Pages/default.aspx#/=

Social Work Practice in Schools retrieved from: https://www.caswacts.ca/en/social-work-practice-schools

Student Code of Conduct retrieved from: http://www.prsdmb.ca/studentcode-of-conduct/

Study Tips retrieved from: https://kidshealth.org/en/teens/center/homework-help.html#catstudysmart

The Newcomer's Guide to Elementary School in Ontario retrieved from: https://settlement.org/ontario/education/elementary-and-secondary-school/newcomers-guides-toeducation/the-newcomer-s-guide-to-elementaryschool-in-ontario/

The Newcomer Guide to Schooling in Canada retrieved from: https://arrivein.com/studying/thenewcomer-guide-to-schooling-in-canada/

The Official BRC Survival Guide retrieved from: https://www.spsd.sk.ca/school/bedfordroad/Abou t/handbook/Documents/handbook20.pdf

Tips for Parents retrieved from: https://peopleforeducation.ca/wpcontent/uploads/2017/07/Parent-Involvement-English.pdf

West Vancouver Secondary School Code of Conduct retrieved from: https://westvancouverschools.ca/westvancouversecondary/about-wvss/code-of-conduct/

Why does Alberta still have a separate Catholic school system? Here's a 2 minute explanation retrieved from: https://www.cbc.ca/news/canada/calgary/whyalberta-saskatchewan-ontario-have-separatecatholic-schools-1.4614462

ADDRESS:
104-407 LUDLOW STREET
SASKATOON, SK S7S 1P3
CANADA
WEBSITE ADDRESS:
HTTP://WWW.SAISIA.CA